

**KUMBUKIZI YA ‘BABA WA KISWAHILI’
MOHAMED HASSAN ABDULAZIZ MKILIFI**

Novemba 11, 1932 – Julai 10, 2023

ENOCK MATUNDURA & PATRICK IRIBEMWANGI



Picha iliyohaririwa imetumiwa kwa idhini ya Nation Media.

Mnamo Julai 10, 2023, taaluma ya Kiswahili ilipata pigo kubwa kutokana na kifo cha Prof Mohamed Hassan Abdulaziz “Mkilifi”, ambaye alifunza isimu katika vyuo vikuu mbalimbali ulimwenguni kwa zaidi ya miaka hamsini. Prof Abdulaziz ambaye alifariki akiwa na umri wa miaka 91 alitambuliwa kwa lakabu ya ‘baba wa Kiswahili’. Lengo la makala hii ni kumuenzi msomi huyu kwa mchango wake katika taaluma ya Kiswahili kama mtaalamu aliyeweka msingi imara wa taaluma ya Kiswahili Afrika Mashariki na kwingineko, kwa kuwalea na kuwakuzwa wataalamu wengine aliowafundisha moja kwa moja katika viwango mbalimbali, kuwasimamia katika shahada za uzamili na uzamifu na kwa kazi nyingi za kitaaluma alizoziandika. Aidha ni muhimu kutaja kwamba hulka na mchango wa Mohamed Hassan Abdulaziz katika taaluma za Kiswahili inaweza kuelezwa na kufafanuliwa kwa mikabala mbalimbali. Inachukua mkondo wa

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

kisa cha vipofu sita waliogusa sehemu mbalimbali za mwili wa ndovu, na kila mmoja akaeleza jinsi alivyoifasiri sehemu aliyoigusa. Kwa hiyo, makala hii ni mtazamo wa waandishi na wataalamu wengine kumhusu Mohamed Hassan Abdulaziz. Tumeegemea wasifukazi wake na taarifa zilizowahi kuchapishwa kumhusu, maoni ya wataalamu wengine na hata kauli zake (M. H. Abdulaziz) mwenyewe, zilizofumbatwa kwenye mahojiano na wataalamu wengine.

Kuzaliwa, Elimu na Kazi ya Mohamed Hassan Abdulaziz

Mohamed Hassan Abdulaziz (Mkilifi) alizaliwa Novemba 11, 1932 mjini Mombasa, Kenya. Wazazi wake walikuwa ni Bw. Hassan Abdulaziz na Bi. Mwana Nana wa Omari¹. Alianza masomo yake ya awali ya Cambridge School katika Mombasa School (1940-1949) ambapo alijipatia cheti cha Cambridge School Certificate (CSC). Baadaye alipata mafunzo ya ualimu katika Coast Teacher Training College, Mombasa (1952-1954), na kupata hati ya Primary School Teacher's Certificate (PSTC), na akawa mwalimu wa shule ya msingi.

Katika miaka ya 1957 na 1958 alikuwa Mwalimu Mkuu Mshikilizi katika Shule ya Sir Ali Bin Salim katika eneo la Malindi. Baada ya kufuzu na shahada ya kwanza, M.H. Abdulaziz alifanya kazi kama mwalimu katika Shule ya Upili ya Khamis. Katika wakati huo pia (1963-1967), M. H. Abdulaziz pia alihudumu kama Afisa wa Elimu.

Baadaye alipata ufadhili wa kwenda kusoma katika School of Oriental and African Studies (SOAS), jijini London, Uingereza, ambapo alisomea shahada ya Bachelor of Arts katika taaluma ya Classical and Modern Arabic. Aliendelea na masomo ya uzamili katika chuo hicho na kuandika tasnifu yake kuhusu Ushairi wa Kiswahili wa Kabla ya Karne ya 20, akijikita kwenye mashairi ya mtunzi maarufu wa mashairi, Muyaka Bin Haji al Ghassaniy. M. H. Abdulaziz alikamilisha masomo yake ya shahada ya uzamifu katika chuo hicho kwa kuandika tasnifu kuhusu Sintaksia ya Kiswahili.

Baada ya kupata shahada ya uzamili na stahada ya juu ya Isimu, Prof. Abdulaziz alichukua wadhifa mpya mwaka wa 1967 kama mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, Dar es Salaam alikohudumu mpaka mwaka wa 1970. Katika chuo hicho, alifunza Kiswahili na Isimu na akapanda ngazi kuwa Mhadhiri Mkuu na Kaimu Mwenyekiti wa Idara ya Lugha na Isimu.²

¹ Tunamshukuru Ustadh Abdilatif Abdalla kwa taarifa hizi. Mohamed H. Abdulaziz ameitabaruku kazi yake: *MUYAKA: 19TH Century Swahili Popular Poetry* (1979). Nairobi: Kenya Literature Bureau kwa kumbukizi ya watu wanne: Mwalimu Sikujua, Rev. William E. Taylor, Shihabuddin Chiraghdin, na Mwana Nana wa Omari, ambaye alikuwa mama yake. Muhammad Sikujua (mnukuzi) na Rev. William E. Taylor walimsaidia sana Prof. Abdulaziz wakati wa utafiti wake, na ndio walikuwa wakusanyaji wa kwanza wa mashairi ya Muyaka ambayo yalimfaa sana wakati wa utafiti kuhusu mashairi ya mtunzi huyo.

² Mbali na kufundisha, Abdulaziz alikuwa mhariri wa jarida la *Swahili* kuanzia mwaka 1968, baada ya J.W.T. Allen kuondoka.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

Baadhi ya wataalamu aliofunza nao ni Prof. Wilfred Whiteley, Prof. John Woodhead na Prof. Farouk Topan. Baadaye mwaka huo wa 1970, alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi katika Idara ya Fasihi kwa Kiingereza alikofundisha kwa mwaka mmoja. Mwaka uliofuata, Profesa aliiasisi Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Nairobi na akawa Mwenyekiti Mwanzilishi wa Idara hiyo. Alipandishwa ngazi na kuwa Profesa Mwandamizi mnamo 1974 na akahudumu katika nafasi hiyo hadi 1978 alipochukua nafasi ya Profesa aliyoishikilia mpaka alipostaafu na kufikwa na mauti. Kati ya 1971 na 1986, Prof. Abdulaziz alikuwa Mwenyekiti wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika alikoendelea kufunza chini ya wenyekiti tofauti kwa muda wa miaka mingine 26. Katika mwaka wa 2013, Idara ya Kiswahili iliasisiwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi chini ya uenyekiti wa Prof. John Habwe. Profesa Abdulaziz, kama msomi tajika wa Kiswahili, alijiunga na idara hiyo.³

Mohamed H. Abdulaziz kama ‘Baba ya Kiswahili’ na Mwalimu wa Walimu

Lakabu ya ‘Baba wa Kiswahili’ au ‘mwalimu wa walimu’ zilimfaa M. H. Abdulaziz kwa sababu nne kuu. Kwanza alikuwa miongoni mwa wataalamu walioanzisha Idara za Isimu na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Nairobi kama tulivyokwisha kutaja hapo juu. Pili, wanafunzi wengi waliopitia mikononi mwake walikwea ngazi ya taaluma na kuwa ama wasomi wa kutajika au waandishi mahiri wa wa fasihi ya Kiswahili. Tatu, M. H. Abdulaziz alikuwa mdogo wa kimo, mpole, asiyejitakia makuu, na mwenye moyo mkubwa wa kuwasaidia watu wengine. Sifa hizi zilimwezesha kutangamana na kutagusana kwa urahisi na watu wa ngazi na matabaka mbalimbali. Nne, kwa kushirikiana na wataalamu wengine, aliandaa mitaala ya ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Nairobi. Katika kushadidia hulka ya mtaalamu huyu, Iribemwangi (2016) anaeleza:

Unapomwona akiwa kwenye pitapita zake katika vijia na ngazi za Chuo Kikuu cha Nairobi, kamwe huwezi kuambatanisha kiwiliwili chake na sifa alizonazo. Pia, huwezi kuambatanisha kiwiliwili hicho na umri wake. Utafyeka miongo miwili kutoka kwa umri wake pasipo kuhisi kukosea. Mwenyewe hupita kwa kuinamisha uso kama mtu anayeona haya. Daima hupendi kujitweza na humsalimu yeyote anayemsimamisha kwa heshima kubwa. Anapenda mno kujidunisha. Ni mtiifu, mfuata maelekezo na ambaye hutimiza wajibu wake kwa wakati ufaao pasipo kukumbushwa. Anapozungumza, matao yake huwa ya chini na huepuka na kukaa mbali na migogoro ya aina yoyote ile. Kwenye vikao vya kiusomi, huketi kama ambaye haelewi yanayoendelea, lakini afunuapo kinywa kutoa mchango wake, mawazo anayoyatoa humwacha kila mmoja bila shaka yoyote kuhusu umuhimu wa tajriba pevu na fikra yenye kina. Hufika afisini mwake kila siku asubuhi kabla ya saa moja; jambo ambalo

³ Sehemu za makala hii zilichapishwa mnamo 2018 kama makala yenye anwani “Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz: Mwanaisimu, Mwandishi na Mwalimu wa Walimu” katika Mwita & al. (wahar.). *Isimu na Fasihi ya Lugha za Kiafrika* (Iribemwangi 2018).

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

huenda amelifanya katika miongo iendayo kufikia mitano kwa sasa. Ngazi na vyumba vya jengo la Education Building anavielewa kuliko kila mmoja wetu idarani kwa sasa. Huyu ndiye Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz aliyezaliwa kisiwani Mombasa tarehe 11 Novemba, 1932.⁴

Baadhi ya wataalamu aliowalea katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni pamoja na Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi (marehemu), Ruth Mfumbwa Beshu (marehemu), Clement Maganga, Mugyabuso M. Mulokozi, Abud Hamisi, Austin Bukenya, David P. B. Massamba (marehemu), Kulikoyela K. Kahigi, Abdu Mtajuka Khamisi (marehemu), miongoni mwa wengine. Kwenye mahojiano na Naomi Shitemi (marehemu) mnamo 2009 katika ofisi yake, Chuo Kikuu cha Nairobi, Abdulaziz anasema:

[...] Idara zote sisi tulikuwa tunakihimiza Kiswahili [...] Na sisi tukaungana kuunda maneno yale ya *curriculum* ya elimu katika upande wa Bayolojia, Upande wa Hisabati [...]. Tukafanikiwa sana, na hapo hapo ikafanywa idara ya Kiswahili na tukapata wanafunzi hodari, maanake katika hawa wanafunzi wetu, ikawa Ebrahim Hussein, (Euphrase) Kezilahabi, (Ruth) Beshu, Mganga (Maganga), Mulokozi, Ndyanao Balisidya (Matteru), Penina Muhando (Mlama)... Wao pia walikuwa na ari, wakapata misingi ile ya kiakademia ya fasihi, n.k. Kezilahabi akawa na digrii yake, akapata PhD. Ebrahim Hussein akapata digrii yake. Akaenda Ujerumani, akasomea PhD katika habari ya drama. Akawa ni wa kwanza kutoa drama [...] Wakatoa fasihi ambazo mtu anaweza akachukulia ni fasihi za kilimwengu. Mimi aliniambia Profesa wa Finland kwamba, fasihi ya Kiswahili ilikuwa sasa ni fasihi ya kilimwengu – yaani *World Literature*. Kwa sababu ina kiwango cha juu sana katika habari za wahusika, habari za ploti n.k. Sasa hayo yalikuwa ni matokeo ya idara zile.⁵

Baadhi ya tungo maarufu za kidrama alizoandika Ebrahim Hussein ni pamoja na *Kinjeketile* (1969), *Mashetani* (1973), *Jogoo Kijijini/Ngao ya Jadi* (1976), *Arusi* (1980), *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988) miongoni mwa kazi nyingine. Kwa upande mwingine, Euphrase Kezilahabi, ambaye alifariki mnamo 2020, aliondokea kuwa mwandishi wa riwaya na ushairi wa kimapinduzi. Riwaya zake *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), na diwani zake za mashairi kama vile *Kichomi* (1974), *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008) zilimdhahirisha kama mwanamapinduzi ambaye aliipanua na kuisogeza mipaka ya fasihi ya Kiswahili. Ndyanao Balisidya (Matteru) naye alitunga riwaya ya *Shida* (1975) naye Penina Muhando akaandika tamthilia za *Nguzo Mama* (1982) na *Lina Ubani* (1984).

Alipoondoka katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kujiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi mnamo 1970 baada ya kugawika kwa Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, M. H. Abdulaziz alishirikiana na wataalamu wengine kama Bernd Heine (kutoka Cologne, Ujerumani) kuandaa

⁴ Rej. hotuba iliyotolewa na Mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi, Prof. Iribemwangi, mnamo Oktoba 2016 kwenye hafla ya kumuenzi Prof. M. H. Abdulaziz iliyofanyika Mombasa, Kenya.

⁵ Taz. Shitemi 2011: 157-172.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

mtaala na kuanzisha Idara ya Isimu na Lugha Nyingine za Kiafrika katika chuo hicho. Abdulaziz katika Shitemi (2011: 160) anasema:

Katika mwaka wa sabini, tukawa na ile East African University ikavunjika. Tukawa na *National Universities*. Tukawa tuna yetu Nairobi, wao yao ya Dar es Salaam, na Waganda yao ya Makerere. Mimi nikarudi nyumbani katika mwaka wa sabini. Nikaanzisha idara ya Linguistics na African Languages. Mimi peke yangu na wanafunzi sita. Siku zile hatukuweza kuiita idara ya Kiswahili maanake kulikuwa na upinzani mkubwa sana kutoka kwa wakubwa wale. Kama Mkuu wa Sheria, yule [...] kama tungeiita Idara ya Kiswahili hawangekubali. Sasa tukaiita ‘Linguistics and African Languages’. Nikawaita watu wa kutoka nje kama Bernd Heine [...] Wajerumani wakaja kutusaidia, tukaanza kufanya ile *curriculum* ya Kiswahili. Ile *Swahili usage* [...]. Katika wakati ule, tukafanikiwa, tukapata wanafunzi wengi wenye ari. Mwanafunzi wangu wa kwanza aliyefanya masters ni Profesa Chacha Nyaigotti Chacha. Kisha tukawa na PhD *programmes*, Wanafunzi kama Okoth (Okombo), wakafanya masomo mengine. Kitsao (Jay) wakafanya Kiswahili. PhD yao mimi nilisimamia, Bakari (Mohamed) [...]. Hawa wakachangia kukileta Kiswahili katika hali ya juu. Tukapigana kuwa katika chuo kikuu, Kiswahili kifundishwe katika Kiswahili.

‘Kupitia katika mikono yake’ ni dhana tunayoitumia katika makala hii kumaanisha kwamba, ama aliwafundisha au kusimamia tasnifu zao za uzamili na uzamifu. Baadhi ya wataalamu ambao Mwalimu M. H. Abdulaziz aliwasimamia ni pamoja na Maprofesa Lucia Omondi, Karega Mutahi, Chacha Nyaigotti-Chacha, Okoth Okombo (marehemu), Mohamed Bakari, Jay Kitsao (marehemu), Kithaka wa Mberia, Kineene wa Mutiso, John Habwe, Mwenda Mbatiah, Rayya Timammy, Obuchi Mosei na Ayman Al-Azhar. Wengine ni Madaktari Isaiah Ndung’u Mwaniki, Ayub Mukhwana, Jefwa Mweri, Justin Sikuku na Mohamed Majid Akidah. Mbali na wataalamu hawa wa nchini Kenya, Profesa pia amesimamia wanafunzi kutoka nchi nyingi za nje zikiwemo Marekani, Kanada, Bara Uropa, Japan, Korea, Saudi Arabia na Misri. Kizazi hiki cha wataalamu waliopitia katika mikono ya mwalimu M. H. Abdulaziz katika vyuo vikuu vya Nairobi na Dar es Salaam kiliwapokeza mwenge wa ukuzaji na ustawishaji wa wa Kiswahili kizazi kingine cha wataalamu. Katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa mfano, kina Jay Kitsao (marehemu), Okoth Okombo (marehemu), Mohamed Bakari waliwafundisha wataalamu wengine ambao sasa ni maprofesa katika taaluma ya Kiswahili. Baadhi yao ni Kimani Njogu, Clara Momanyi, Catherine Ndungo, John Hamu Habwe, Rayya Timammy, Mwenda Mbatiah, Iribe Mwangi, miongoni mwa wengine.

Katika kumuomboleza mwalimu wake kwenye makala katika *Saturday Nation*, July 15, 2023 yenye mada, ‘*The Waswahili celebrating their language and mourning their guru*’, Austin Bukenya anasema:

Finally, please, join me in mourning and honoring our great Mswahili patriarch, Prof Mohamed Hassan Abdulaziz, who passed away last Monday, July 10. I guess, no one even vaguely aware of African Linguistics and Kiswahili studies needs elaborate introduction to Mohamed Abdulaziz, “Mkilifi”. Though arguably the humblest of people I have met in my long life, this quiet-spoken and sometimes stammering man

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

has dominated East African language for more than half a century. He was one of my most trusted advisors and mentors. He taught me linguistics, and introduced me to Kiswahili literature, in the 1960s, at Dar es Salaam University, before he relocated to UoN to start the department of Kiswahili (sic) and African Languages. [...] I do not think that even Prof Abdulaziz himself could count the number of students he taught, or supervised, at every level of scholarly study, in his unique career. Though originating in the Swahili community of Kilifi, hence the moniker “Mkilifi”, he spent most of his early working life in Mombasa, which explains his strong interest in Kimvita poetry. For a gentle, polished, cultured, generous Mswahili, I point to Mwalimu Mohamed Abdulaziz. Mola amlaze mahali pema peponi.

Mwisho, nakuomba, ujiunge nami katika kumuomboleza na kumuenzi baba yetu Mswahili, Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz, aliyefariki Jumatatu iliyopita, Julai 10. Nimaamini, hakuna mtu yeyote, hata yule anayejua machache sana kuhusu Isimu ya Kiafrika na masomo ya Kiswahili, anahitaji utambulisho wa kina wa Mohamed Abdulaziz, “Mkilifi”. Ingawa kwa hakika ni mmoja wa watu wanyenyekevu zaidi niliowahi kukutana nao maishani mwangu, mtu huyu, mnyamavu na wakati mwingine anayesema kwa kigugumizi amechangia na kuvuma sana kwenye ulingo wa taaluma ya lugha Afrika Mashariki kwa zaidi nusi karne. Alikuwa mmoja wa washauri wangu niliowaamini, Alinifundisha Isimu, na kuniingiza katika Fasihi ya Kiswahili, katika miaka ya 1960, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kabla ya kuguria Chuo Kikuu cha Nairobi kuanzisha Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika. [...] Sifikiri kwamba, hata Prof Abdulaziz mwenyewe anaweza kuhesabu idadi ya wanafunzi aliowafundisha, au kusimamia, katika kila kiwango cha usomi katika taaluma yake yenye upekee. Ingawa asili yake ni jamii ya Wakilifi, Uswahilini, na hiki ndicho chanzo cha lakabu yake “Mkilifi”, alikaa eneo la Mombasa kwa muda mrefu ambako alifanya kazi, nah ii ndiyo labda sababu alivutiwa sana na ushairi wa Kimvita. Kwa mtu mpole, muungwana, mstaarabu, mkarimu, kielelezo bora cha Mswahili, ni sifa ninazompa Mwalimu Mohamed Abdulaziz. Mola amlaze pema peponi. (Tafsiri yetu).

Kutokana na maoni na mitazamo ya wataalamu wengine kumhusu M. H. Abdulaziz, hatukosei kudai kwamba tunapotathmini mikondo ya usomi ya Kiswahili Afrika ya Mashariki katika kipindi cha miongo mitano ambayo mwalimu M. H. Abdulaziz alifundisha, alama za nyayo alizoziacha hazikosi kudhihirika wazi. Kwa mafano, kwenye kongamano lililoandaliwa na Chama cha Kiswahili cha Taifa, Kenya (CHAKITA) mnamo 2016 kumuenzi mtaalamu huyu (M. H. Abdulaziz), kwa mchango wake katika maendeleo ya Kiswahili, ilibainika kwamba wajumbe wote waliohudhuria hafla hiyo walikiuwa ama ni wanafunzi wake wa zamani, au wanafunzi wa wanafunzi wake, au wanafunzi wa wanafunzi wa wanafunzi wake, n.k. Katika kushadidia mchango wa M. H. Abdulaziz katika taaluma ya Kiswahili, Mulokozi (2019: 23) anasema:

Historia ya kuanzishwa kwa taaluma halisi ya lugha na fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania (na Afrika Mashariki) itakapoandikwa, Majina ya Prof. Mohamed Abdulaziz na Profesa Farouk Topan sharti yatajwe kwa adhama. Wataalamu hao, mmoja kutoka Kenya (Abdulaziz) na mwingine kutoka Zanzibar (Topan) ndio waanzilishi wa taaluma za Kiswahili katika CKKD⁶ katika mwaka wa masomo 1967/68.

⁶ Herufi CKKD zinasimamia Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

Katika kuisitiza misingi imara katika taaluma ya Kiswahili na athari zake, Mulokozi (2019:25) anaeleza taswira ya ‘upokezanaji kigongo’⁷ katika taaluma ya Kiswahili ambacho kitovu chake kinaanzia kwa wataalamu wawili; yaani Abdulaziz na Topan. Anasema kwamba, Abdulaziz na Topan walifundisha wataalamu wa mwanzo wa lugha ya Kiswahili (k.m. Ebrahim Hussein, Penina Muhando, Ndyanao Balisidya); wataalamu hao wakafundisha ‘kizazi cha’ pili (Sengo, Kiango, Mulokozi, Kahigi, Madumulla). Mulokozi anaendelea kusema kuwa ‘kizazi’ cha tatu kilichofundishwa na kile cha pili ni akina Said A. Mohamed, Abel Gibbe, Emmanuel Mbogo, Mohamed Seif Khatib, Ibrahim Ngozi. Anadai kuwa hiki kizazi cha tatu ndicho kwa kiasi kikubwa kilikuja kuasisi na kuendeleza masomo ya Kiswahili katika vyuo vikuu vingi nje ya Tanzania kama vile Japan, Korea, Marekani, Uchina, Libya, Sudan, Burundi, Rwanda na Kenya kuanzia miaka ya 1980 na kuendelea.

Taswira anayoichora Mulokozi inaturejesha pale pale kwenye kauli yake kwamba itakapoandikwa historia ya maendeleo ya taaluma ya Kiswahili si Afrika Mashariki tu, bali kote ulimwenguni, majina ya M. H. Abdulazi na Farouk Topan yatatajwa kwa heshima kubwa. Kwa hiyo, hatua za M. H. Abdulaziz kuanzisha idara za Kiswahili kwa ushirikiano na wataalamu wengine nchini Kenya na Tanzania, kuwafundisha na kuwalea wataalamu wengine walioibuka kutoa michango mikubwa katika fasihi na isimu ya Kiswahili, na machapisho ya makala na vitabu mbalimbali kuhusu taaluma ya Kiswahili ni juhudi zinazohalalisha lakabu alizopewa, yaani ‘Mwalimu wa Walimu’ na hata ‘Babu wa Kiswahili’ Afrika ya Mashariki.

Tafakuri ya Abdulaziz kuhusu Uwezo na Mustakabali wa Kiswahili na Lugha za Kiafrika

M. H. Abdulaziz alikuwa msomi na mwanaharakati aliyezienzi kwa dhati lugha za Kiafrika, hususan Kiswahili. Aliamini kwamba, Kiswahili kina uwezo wa kutumika katika kufundishia masomo yoye yakiwemo ya sayansi. Alipohudumu katika Chuo Kikuu cha Nairobi, alipigania kubadilishwa kwa sera ya chuo hicho iliyosisitiza Kiingereza kiwe lugha rasmi ya pekee. Mmoja wa wanafunzi wake kipindi hicho, alisimama kidete kupinga sera hiyo. Akizungumzia suala hili, Abdulaziz katika Shitemi anasema:

Tukapigana kuwa katika chuo kikuu [cha Nairobi], Kiswahili kifundishwe katika Nairobi. Hapa Nairobi ikawa upinzani mkubwa – *language policy* ya *University* hii ilikuwa *official language* ni Kiingereza. Huyu Chacha akaja. Naye ni mtu mshindani! Akasema, “Lazima niandike [tasnifu ya] Kiswahili katika lugha ya Kiswahili!” Ikawa lazima twende mpaka Senate kukubaliwa ya kwamba mtu anaweza kuandika tasnifu katika lugha ya Kiswahili!

⁷ Dhana ya ‘kupokezana kigongo’ inanuiwa kufumbata fahiwa ya mashindano ya mbio ambapo kundi la wanariadha hukimbia kama timu moja, ambapo mwanariadha mmoja hukimbia akiwa ana kigongo/kijiti mkononi. Anakimbia masafa yake na kumpokeza mwenzake, ambaye pia hukimbia na kumpokeza mwingine. Katika taaluma ya Kiswahili, M. H. Abdulaziz na Farouk Topan waliwafundisha kina Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi n.k. Mulokozi ametumia dhana ya ‘kizazi’ (*generation*) kuelezea dhana hii.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

Chacha akaandika, [akawa] wa kwanza kuandika MA [tasnifu]⁸ katika Kiswahili kwa Kiswahili. Na ile ikafungua milango, sasa ikawa MA zote zinaandikwa kutumia Kiswahili. Lakini sasa, bahati mbaya hatujakubaliwa tufanye PhD.⁹ Abdulaziz anasema kuwa Kiswahili kina msamiati wa kutosha sasa wa kufundisha fasihi ya Kiswahili na Isimu kwa Kiswahili.

Mtaalamu huyu aliamini kwamba Waafrika wanaweza kujikomboa kutokana na ukoloni-mamboleo kwa kutilia maanani lugha na tamaduni zao na pindi hali hiyo itakapotimia, Waafrika wataonekana kuwa wao pia ni wanadamu katika dunia wenye utamaduni wao, miziki yao ambazo sasa zimegandamizwa kwa sababu ya kuharibu lugha ile rasmi na kuthamini lugha za Kigeni. Hivi ndivyo alivyomweleza Shitemi:

Mtu anaweza akaandika leo juu ya jambo lolote la isimu kama fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki katika Kiswahili. Na hayo kwangu mimi ni mafanikio makubwa sana. Na ni mafanikio ambayo sote tumechangia [...] Wengine kama Thailand, Indonesia, China wamefanikiwa. Majapani walianza katika karne ya kumi na nane kukifanya Kijapani lugha ya kitaifa. Unaweza kufanya masomo yote, mambo ya tonoradi (*nuclea*), katika lugha hii. Na sisi hapa tulipofika sasa, tumefika mahali wanapoita Waingereza ‘*a take-off point*’. Tukipata msukumo ule wa kiserikali tunaweza kushirikiana sote katika idara zetu na mabingwa wote tukatoa misamiati katika fani zote kama walivyofanya Majapani na watu wa Thailand na hiki Kiswahili kikatumika katika nyanja zetu zote.

Michango ya M. H. Abdulaziz, Tuzo alizopata na Machapisho Yake

Katika uhai wake, M. H. Abdulaziz alishiriki kwenye warsha na makongamano na mikutano mingi ambapo alitwikwa majukumu ya kuwa Mwasilishi Mkuu. Jukumu hili alilitekeleza katika makongamano na mikutano mingi katika pembe mbalimbali za dunia. Mialiko hiyo ilitokana na tajriba na ujuzi wake uliosambaa ulimwenguni kote. Juu ya hayo, ana machapisho chungu nzima. Dhana ya *triglossia*¹⁰ aliyoitumia mnamo mwaka wa 1972 katika makala “Triglossia and Swahili-English Bilingualism in Tanzania” kuelezea hali ya lugha barani Afrika sasa inatumiwa katika takriban kila chapisho la isimujamii. Kufikia sasa, ni vigumu msomi wa Kiswahili kuepuka kusoma kitabu chake *Muyaka: 19th Century Popular Swahili Poetry* (KLB, 1979) ambacho kilitokana na usilimisho na upanuzi wa tasnifu yake ya uzamili (MA) aliyoiwasilisha katika The University of London mnamo

⁸ Chacha Nyaigotti-Chacha aliandika tasnifu yake ya uzamili kuhusu ushairi wa Abdilatif Abdalla. Baadaye tasnifu hiyo ilichapishwa kitabu chenye anwani ‘*Sauti ya Utezezi: Ushairi wa Abdilatif Abdalla*’ (Nyaigotti-Chacha 1992). Kazi alizozichunguza ni *Utenzi wa Adamu na Hawaa* (1971) na *Sauti ya Dhiki* (1973).

⁹ Mahojiano haya yalifanyika Novemba 9, 2009. Sasa hivi, Chuo Kikuu cha Nairobi kimebadilisha sera yake na tasnifu za kiwango cha PhD sasa zinaandikwa kutumia Kiswahili. Mwenyekiti wa sasa Prof. Iribe alipigania sana jambo hilo hadi likakubalika mwaka wa 2018. Prof. Abdulaziz ambaye bado alikuwa Idarani alifurahia sana hatua hiyo iliyotimiza azma yake.

¹⁰ Katika taaluma ya isimujamii, dhana ya triglossia inamaanisha hali ya kuwepi kwa lahaja tatu za lugha lakini kila moja yahaja hizo ikiwa na matumizi maalumu. Taz. Massamba 2004: 87.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

Machi, 1966. Mada ya tasnifu hiyo ilikuwa: ‘Analysis of the Swahili Poems of Muyaka bin Haji of Mombasa, 1776-1840.’

Mwalimu M. H. Abdulaziz pia alitunukiwa tuzo chungu nzima za kiusomi na kitaifa kutokana na ujuzi na huduma zake katika uwanja wa elimu. Katika ngazi ya kitaifa, Abdulaziz aliwahi kutunukiwa tuzo ya *Order of the Grand Warrior* (OGW) na Serikali ya Kenya kutokana na huduma yake katika elimu. Fauka ya haya, alipata kuzuru vyuo vikuu vingi duniani¹¹ kama Profesa Mwalikwa alikokutana na kusaidia kitaaluma wanafunzi wengi kutoka Kenya kama vile Prof. K. W. Wamitila na Prof. Jayne Mutiga aliokutana nao katika Chuo Kikuu cha Bayreuth wakiwa wanafunzi wa uzamifu. Alikuwa Bayreuth mara kadhaa ili kuchangia kwenye tafsiri ya tungo za Fumo Liyongo.

Baadhi ya Machapisho ya M. H. Abdulaziz

M. H. Abdulaziz alichapisha sana katika taaluma ya lugha na isimu. Alikuwa mwanachama wa asasi nyingi kuu za kimataifa kuhusu lugha na alihudumu katika bodi nyingi za uhariri wa majarida. Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya machapisho yake ya vitabu na makala za kitaaluma.

Vitabu na Matoleo ya Jarida

1979. *Muyaka. 19th Century Popular Swahili Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
1986. (with Joshua A. Fishman, Michael Clyne, Andrée Tabouret-Keller & Bhadriraju Krishnamurti; eds.). *The Fergusonian Impact. In Honor of Charles A. Ferguson on the Occasion of his 65th Birthday*. Volume 1: From Phonology to Society & Volume 2: Sociolinguistics and the Sociology of Language. Berlin & New York: Mouton de Gruyter. 1.743 pp.
1996. *Transitivity in Swahili*. Cologne: Rüdiger Köppe.
- 1997 (issue editor). Sociolinguistic Issues in Sub-Saharan Africa. *International Journal of the Sociology of Language* 125. Berlin & New York: Mouton De Gruyter.
- 2004 (with Gudrun Mieke, Abdilatif Abdalla, Zeina Al-Bakary, Angelica Baschiera, Ahmad Nassir Juma Bhalo, Clarissa Dittermer, Said Ahmed Mohamed Khamis, Ahmed Nabahany, Yahya Ali Omar & Farouk Topan, wahar.). *Liyongo Songs. Poems Attributed to Fumo Liyongo*. Cologne: Rüdiger Köppe.

¹¹Alizuru vyuo nchini Marekani, Mashariki ya Kati, Ulaya na Afrika, mbali na kuhudhuria makongamano mengi katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. M. H. Abdulaziz aliwahi pia kuhudumu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Sayansi za Kijamii ya Tume ya Kitaifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Alikuwa pia mwanachama mwanzilishi wa Akademia ya Sayansi ya Kenya (Kenya National Academy of Sciences, KNAS) ambapo alipata kiwango cha juu kabisa kama “Fellow” (FKNAS)

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

Makala na Sura za Vitabu

1968. A Note on the Form and Language of the Poem. Hasani Bin Ismail. *The Medicine Man – Swifa ya Nguvumali*. Edited and translated by Peter Lienhardt. Oxford: Clarendon Press. pp. 81-83.
1971. Tanzania's National Language Policy and the Rise of Swahili Political Culture. Wilfred H. Whiteley & Darryl Forde (Eds.). *Language Use and Language Change. Problems of Multilingualism with Special Reference to Eastern Africa*. London: OUP. pp. 160-178.
1972. Trilingualism and Swahili-English Bilingualism in Tanzania. *Language in Society* 1: 197-213.
1977. (with Mohamed Hyder). Language Situation in Kenya. Alfa Ibrahim Sow (ed.). *Langues et politiques de langue en Afrique Noire. L'expérience de l'UNESCO*. Paris: Éditions NUBIA. pp. unknown.
1979. Methodology of Sociolinguistics Surveys: The East African Language Survey Experience. *Journal of Eastern African Research and Development* 9 (1&2): 1-27.
1980. The Ecology of Tanzanian National Language Policy. Edgar C. Polomé & Charles P. Hill (eds.). *Language in Tanzania*. London & Oxford: International Africa Institute & OUP. pp. 139-175.
1982. Patterns of Language Acquisition and Use in Kenya: Rural-Urban Differences. *International Journal of the Sociology of Language* 34 (1982): 95-120.
1983. (with Paul Otto Samuelsdorff). Semantic Analysis of Swahili Applicative Extension. A Functional Approach. Sandor Rot (ed.). *Languages in Function*. Budapest: MTA. pp. 21-31.
1984. Aspects of Lexical and Semantic Elaboration in the Process of Modernization of Swahili. Joan Maw & David Parkin (eds.). *Swahili Language and Society. (Beiträge zur Afrikanistik 23)*. Wien: Afro-Pub. pp. 195-213.
1986. Factors in the Development of Modern Arabic Usage. *The International Journal of the Sociology of Language* 62: 11-24.
1988. A Sociolinguistic Profile of East Africa. Ulrich Ammon, Norbert Dittmar & Klaus J. Mattheier (Eds.). *Sociolinguistics. An International Handbook of the Science of Language and Society*. Volume 1.2. Berlin & New York: Walter de Gruyter. pp. 1347-1353.
1991. East Africa (Tanzania and Kenya). Jenny Cheshire (ed.). *English around the World: Sociolinguistic Perspectives*. Cambridge: Cambridge University Press. pp. 389-401.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

1991. Language in Education: A Comparative Study of the Situation in Tanzania, Ethiopia and Somalia. Ofelia García (ed.). *Focus on Bilingual Education. Essays in Honor of Joshua A. Fishman*. Volume 1. Amsterdam: John Benjamins. pp- 75-86.
1993. Language Use and Language Development: Review of Sociolinguistic Theory. William A. Foley (ed.). *The Role of Theory in Language Description. (Trends in Linguistics – Studies and Monographs 69)*. New York: Mouton de Gruyter. pp. 421-436.
1993. (with Alfa Ibrahim Sow). Language and Social Change. Ali A. Mazrui (ed.). *UNESCO General History of Africa. Volume VIII: Africa since 1935*. Nairobi, Oxford & Paris: East African Educational Publishers, James Currey & UNESCO Publishing. pp. 522-552.
1993. History of the Spread of Islam on the East African Coast. Konrad-Adenauer-Stiftung (ed.). *Islam in Africa South of the Sahara*. Sankt Augustin: Konrad-Adenauer-Stiftung. pp. unknown.
1995. Kulinganisha na Kulinganua Toleo la Sasa Na Mswada wa Toleo Jipya. Hermas J.M. Mwangi & Albina R. Chuwa (wahar.). *Tahakiki Na Uchapishaji wa Kamusi*: Dar es Salaam: TUKI. pp. 19-28.
1995. Impact of Islam on the Development of Swahili Culture. Mohamed Bakari & Saad S. Yahya (eds.). *Islam in Kenya*. Nairobi: MEWA Publications. pp. 142-157.
1996. The Influence of the Qasida on the Development of Swahili Rhymed and Metred Verse. Stefan Sperl & Christopher Shackle (eds.). *Qasida Poetry in Islamic Asia and Africa*. Leiden / New York: Brill. pp. 411-428.
1997. (with Ken Osinde). Sheng and English: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya. *International Journal of the Sociology of Language* 125: 43-63.

Marejeleo

- Abdulaziz, Mohamed Hassan. 1979. *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Bukenya, Austin Lwanga. 2023. 'The Waswahili celebrating their Language and mourning their Guru'. *Saturday Nation*, 15 July 2023. Nairobi: Nation Media Group.
- Iribemwangi, Patrick. 2018. Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz: Mwanaisimu, Mwandishi na Mwalimu wa Walimu. Leonard Chacha Mwitia, Mosol Kandagor, Sheila Ali Ryanga & Joseph Nyehita Maitaria (wahar.). *Isimu na Fasihi ya Lugha za Kiafrika. Kwa Heshima ya Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz*. Eldoret: Moi University Press. pp. v-viii.
- Massamba, David P. M. 2004. *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

KUMBUKIZI YA MOHAMED H. ABDULAZIZ

- Matundura, Enock. 2023. Prof Mohamed Abdulaziz: The Father of Kiswahili. *Saturday Nation*, 15 July 2023. Nairobi: Nation Media Group. <https://nation.africa/kenya/life-and-style/weekend/prof-mohamed-abdulaziz-the-father-of-kiswahili-4303690>
- Matundura, Enock. 2023. Wataalamu wamuomboleza ‘Baba wa Kiswahili’ Profesa Mohamed Abdulaziz Mkilifi. *Taifa Leo*, Julai 20, 2023. Nairobi: Nation Media Group. uk. 16.
- Mulokozi, Mugyabuso Mlinzi. 2019. Pambazuko la Taaluma ya Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki: 1968-1980. Flavia Aiello & Roberto Gaudio (Wah.). *LUGHA NA FASIHI: Essays in Honour and Memory of Elena Bertoncini Zubkova*. Napoli: Università degli Studi di Napoli “L’Orientale”. uk. 19-31.
- Mwangi, Iribe. 2023. Bado twaomboleza Prof Abdulaziz: Mwandishi na Mwalimu wa Walimu’. *Taifa Leo*, Julai 20, 2023. Nairobi: Nation Media Group. uk. 16.
- Nyaigotti-Chacha, Chacha. 1992. *Sauti ya Utetezi: Ushairi wa Abdilatif Abdalla*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Raia, Annachiara. 2023. *Kwaheri, Baba yetu wa Kiswahili. A Goodbye to the Father of Swahili and African Linguistics, Mohamed Hassan Abdulaziz (1932-2023)*. Leiden: African Studies Centre. <https://www.ascleiden.nl/content/library-weekly/mohamed-hassan-abdulaziz-1932-2023>
- Rajab Ahmed. 2023. Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz: Mswahili aliyetambulika kimataifa kuwa gwiji wa isimu. *Gazeti la Dunia*, 19 Julai 2023. <https://gazetiladunia.com/profesa-mohamed-hassan-abdulaziz-mswahili-aliyetambulika-kimataifa-kuwa-gwiji-wa-isimu/>
- Shitemi, Naomi Luchera. 2011. *Kubidhaaisha na Kuwezesha Lugha Kama Sarafu ya Kiuchumi na Kijamii: Kielelezo cha Taaluma za Kiswahili na Tafsiri*. Eldoret: Moi University Press.